RIPOTI YA KAMATI YA KUDUMU YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA BARAZA LA WAWAKILISHI- KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

SEHEMU YA KWANZA

UTANGULIZI.

Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi imeundwa kwa mujibu wa kifungu cha Kanuni ya **106 (f)** cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo la mwaka 2012 na majukumu yake yametajwa katika kifungu cha (**113)** kama ifuatavyo:

a) Kufuatili utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwenye ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia
b) Kufuatilia utekelezai wa Sera na Mipango ya Wizara husika kwa kadri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji Bajeti na Hotuba nyengine za Waziri alizotoa Barazani.
c) Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na Miradi ya Wananchi ya Wizara husika.
d) Kuchunguza na kufuatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha.
e) Kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka.
f) Kushughulikia Miswada ya Sheria itakayokabidhiwa kwake na Spika.
g) Kuchambua ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufuatilia utekelezaji wa ahadi hizo.
h) Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.

Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa mwaka wa fedha 2014/2015 ilianza shughuli zake za kufuatilia utekelezaji wa kazi za maendeleo ya wizara zifuatazo:

- Wizara ya Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ
- Wizara ya Nchi (AR) Kazi na Utumishi wa Umma
- Wizara ya Katiba na Sheria

Kamati ilifanya kazi zake kwa muda wa wiki nne

i) Pemba wiki mbili tarehe 08/12/2014 hadi tarehe 19/12/2014.
ii) Unguja wiki mbili tarehe 02/02/2015 hadi tarehe 13/02/2015.

Napenda kuchukua nafasi hii adhimu kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa mashirikiano yao ambayo yamewezesha kufanya kazi zetu kwa ufanisi mkubwa. Wajumbe wenyewe ni hawa wafuatao:

1. Mhe. Ussi Jecha Simai - Mwenyekiti
2. Mhe. Abdalla Juma Abdalla - Makamo M/ kiti
3. Mhe. Bikame Yussuf Hamad - Mjumbe
4. Mhe. Nassor Salim Ali - Mjumbe

5. Mhe. Suleiman Hemed Khamis - Mjumbe
6. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Mjumbe
7. Ndg. Aziza Waziri Kheir - Katibu
8. Ndg. Khamis Hamad Haji - Katibu
9.

Kamati ilifanya kazi kwa utaratibu wa kupokea taarifa za utekelezaji wa malengo ya Wizara kwa baadhi ya idara, taasisi au vitengo vya Wizara husika na baadae kukagua baadhi ya sehemu ili kuona hatua zilizofikiwa katika utekelezajiwake.

SEHEMU YA PILI

WIZARA YA NCHI (AR) TAWALA ZA MIKOA NA IDARA MAALUM ZA SMZ

Wizara ya Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ inaundwa na kusimamiwa na Idara na Taasisi zilizogawika katika maeneo makuu manne (4) pamoja na Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba. Idara na Taasisi hizo ni kama ifuatavyo:-

a) IDARA ZA KAWAIDA

1. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;
2. Idara ya Utumishi na Uendeshaji;
3. Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho;
4. Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa; na
5. Idara ya Serikali za Mitaa;

b) MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MIKOA

6. Mkoa wa Mjini Magharibi;
7. Mkoa wa Kaskazini Unguja;
8. Mkoa wa Kusini Unguja;
9. Mkoa wa Kaskazini Pemba;
10. Mkoa wa Kusini Pemba;

c) MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA

11. Baraza la Manispaa – Unguja
12. Baraza la Mji – Wete;
13. Baraza la Mji – Mkoani;
14. Halmashauri – Wilaya ya Magharibi.
15. Halmashauri – Wilaya ya Kaskazini ‘A’.
16. Halmashauri – Wilaya ya Kaskazini ‘B’.
17. Halmashauri – Wilaya ya Kati Unguja.
18. Halmashauri – Wilaya ya Kusini Unguja.
19. Halmashauri – Wilaya ya Wete.
20. Halmashauri – Wilaya ya Micvheweni.
21. Halkmashauri – Wilaya ya Chake Chake.
22. Halmashauri – Wilaya ya Mkoani.

d) IDARA MAALUM ZA SMZ

23. Idara ya Uratibu wa Idara Maalum za SMZ;
24. Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ;

25. Kikosi cha Kuzuia Magendo (KMKM);
26. Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU);
27. Idara ya Chuo cha Mafunzo (MFZ);
28. Kikosi cha Zimamoto na Uokozi Zanzibar (KZU);
29. Kikosi cha Valantia Zanzibar (KVZ)

AFISI KUU PEMBA

Afisi Kuu Pemba ni ni kiungo kikubwa katika Wizara hii na nyengine za Serikali ambapo Kamati ilipatiwa maelezo ya kina juu ya majukumu yake pamoja na jinsi inavyosimamia na kuratibu shughuli zote za Wizara.

Kamati katika ziara yake ilipewa tarifa kuwa Afisi ilifuatilia miradi mbali mbali ya maendeleo ikiwemo miradi minne ambayo kupitia idara zilizopangiwa miradi hiyo ambapo utekelkezaji wake unaendelea vizuri kwas asa.

IDARA YA URATIBU WA IDARA MAALUMU ZA SMZ

Idara hii ni kiuno baina ya Wizara na Idara Maalumu za SMZ na taasisi nyengine za Serikali, jukumu lake ni kuratibu na kusimamia kazi za Idara Maalumu kwa kutekeleza sera, sheria na kanuni za idara maalum pamoja na kusimamia vikao vya mahakama ya Rufaa ya Idara Maalum za SMZ.

CHANGAMOTO

Kutopatikana fedha kwa wakati unaostahiki. Kamati ilipotembelea Idara hii imekuta katika robo moja ya mwaka inaingizia kiasi cha shilingi milioni tano tu, fedha ambazo hazitoshi katika kutekeleza malengo ya Idara.

Idara hii inakabiliwa na ukosefu wa usafiri kwa ajili ya kazi za idara.

Ufinyu wa nafasi katika Afisi za Idara.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Idara ya uratibu iwezeshwe kufanyakazi zake kwa kupatiwa fedha wakati kwa mujibu wa malengo ya kibajeti waliyojipangia kila robo ya mwaka.
2. Kamati inashauri Serikaili kutatua changamoto ya usafiri kwa idara ya Uratibu.
3. Idara ipatiwe Afisi yenye nafasi ya Kutosha.

TUME YA UTUMISHI YA IDARA MAALUMU ZA SMZ

Tume ya Utumishi ya Idara Maalumu inajukumu la kusimamia shughuli za uajiri, kuthibitisha ajira, kusitisha na kuachisha kazi pamoja na kupendekeza maslahi ya watumishi wa Idara Maalumu Serikali kwa mujibu wa Katiba na Sheria.

CHANGAMOTO

1. Ufinyu wa bajeti ya Tume kulingana na majukumu yake na kutopatikana fedha hizo kwa wakati.

2. Mishahara midogo ya watumishi wa Idara Maalumu.
3. Afisi za Tume haziendani na uhalisia wa chombo chenyewe. Kamati imekuta afisi ipo katika eneo finyu ambalo Katibu wa Tume anatumia eneo moja dogo na katibu muhutasi pamoja na watendaji wengine.
4. Upungufu wa vitendea kazi kama vyombo vya usafiri na uhaba wa vifaa vya ofisini.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inashauri Tume kuhakikisha inasimamia kikamilifu zoezi la ajira badala ya kuachia taasisi nyengine.
2. Kamati inaishauri Serikali kurejesha utaratibu wa nyongeza ya kila mwaka kwa watumishi wa Idara Maalumu 'increament' ili kutofautisha baina ya waajiriwa wanaotangulia kuingia kazini na waajiriwa wapya.
3. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha watumishi wa idara maalumu wanakuwa na ngazi za mishahara (salary scales) kwa ajili ya maaskari tu na wasichanganywe na watumishi wa kiraia kwani ni utaratibu katika nchi nyengine askari wanakuwa na ngazi zao za mishahara.
4. Serikali ifikirie kuiwezesha Tume ya Utumishi ya Idara Maalumu kuwa na fungu lake katika bajeti badala ya kuwa na kasma katika matumizi ya Wizara.
5. Kamati inaiagiza Tume kuchukuwa hatua zidi ya malalamiko ya baadhi ya wafanyakazi wa Chuo cha Mafunzo, Makao Makuu ambao kamati inamashaka kuwa taratibu za kuwapa likizo ya ugonjwa hazikufuatwa kwa mujibu wa sheria.

IDARA YA CHUO CHA MAFUNZO

Idara ya Chuo cha Mafunzo ni miongoni mwa Idara nyeti za Serikali ambazo zinastahiki kupewa kipaumbele cha hali ya juu katika utekelezaji wa majukumu yake. Kamati ilifanya ziara kisiwani Pemba na kupewa taarifa ya utekelezaji wa shughuli za kawaida pamoja na kukagua miradi ya maendeleo ambayo inatekelezwa na Idara kwa sasa. Hata hivyo Kamati haikuridhishwa hata kidogo na hali halisi ilivyo katika Idara ya Chuo cha Mafunzo kutokana na hali duni waliyonayo katika maeneo yao ya kazi pamoja na ukosefu mkubwa wa fedha uliopo ambao unakwamisha shughuli za Idara hiyo kuendelea kama zilivyopangwa.

CHANGAMOTO ZA IDARA

Kamati katika ripoti ya utekelezaji ilikutana na changamoto zifuatazo:

1. Ufinyu wa bajeti n uhaba wa askari wa kulinda maeneo mbali mbali ya kazi hasa katika kambi ya Kengeja.
2. Kutoshirikishwa kikamilifu katika uandaaji wa bajeti ya Idara pamoja na kutojua kiwango halisi cha fedha zilizotengwa kwa upande wa Pemba.Kamati ilielezwa kuwa Idara kwa upande wa Pemba mara nyingi hawashirikishwi katika uandaajiwa bajeti yao na hivyo kupelekea kutojua kiwango halisi cha makadirio ya Idara, kutokana na hali hiyo Kamati imesikitishwa sana na jambo hilo ambalo ni jambio la ajabu kwa Idara kubwa kama hii kufanya kjazi bila kushirikiana.
3. Uchakavu na ubovu wa majengo ya ofisi pamoja na nyumba za kuishi askari na ubovu wa magereza ya wafungwa. Kamati hakiuridhishwa na jinsi hali ya ofisi za Iadara zilivyo kutokana na majengo mengi kuwa machakavu na mabovu na hayafai kukaliwa na

binadamu kwa matumizi ya ofisi. Aidha kamati milikagua katika ofisi za Idara zilizoko Wete na kukagua Afisi ya Kamishna wa Idara hii ambapo ilishangazwa na jinsi hali ya chumba kilivyo kwani ni kidogo sana na hakina nafasi ya kutosha kwa matumiz ya oifisi.

4. Kukosekana kwa kituo cha afya katika kambi hasa ya Kengeja.Kamati katika ziara yakle ilishuhudia ukosefu wa kituo cha afya katika kambi ya Kengeja ambapo wanafunzii katika kituo hicho wanakabiliwa na changamoto ya kukjosa kituo cha afyta pamoja na sehemu nzuri ya kuishi kutokana na jengo walilokuwa wakilitumia mwanzo kuanguka kwa upepo.
5. Pia Kamati ilielezwa kuwa baadhi ya kambi za Idara ya Chuo cha Mafunzo zinakabuiliwa na changamoto ya ukosefu wa hati miliki ikiwemo kambi ya Kengeja.
6. Kamati ilielezwa kuwa idara inakabuiliwa na changamoto ya ukosefu wa usafiri wa uhakika kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Idara za kila siku. Katika kambi ya Kengeja Kamati ilishuhudia usafiri uliokuwepo ambao ni mbovu na sio wa uhakika.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati imesikitishwa sana na hali iliyoikuta kisiwani Pemba hasa katika maeneo ya utekelezaji wa bajeti kutoakana na ukosefu wa fedha na kutojulikana kiwango halisi kinachoingizwa kwa taasisi hii kisiwani humo. Aidha Kamatri imesikitika sana na kiwango cha fedha za OC zinazoingizwa kuwa ni chache sana, Kamati ilipotembelea katika baadhi ya kambi ilipewa taarifa kuwa OC iliyoingizwa ni shilingi laki mbili fedha ambazo hazitosghi kufanyia jambo lolote. Hivyo, Kamati inaiagiza Idara ya Chuo cha Mafunzo kuhakikisha kuwa katika uandaaji wa bajeti inawashirikisha wakuu wa Idara zote waliopo Pemba kikamilifu kwa lengo la kujua kiwango halisi cha fedha zinazoingizwa na fedha hizo zinazotengwa ziingizwe kwa wakati kwa mujibu wa majadiliano yao ya kuandaa bajeti.
2. Kamati inaomba Wizara na Serikali kwa ujumla kuhakikisha kuwa inaweka mazingira mazuri ya kufanyia kazi kwa lengo kuwapa hamasa ya kazi wafanyakazi wake. Hali hii inatokana na hali halisi ya majengo ya ofisi yaliyoko kisiwani Pemba ni machakavu na mabovu na mengine hayakaliki na ni hatari kwa uhai wa binadamu. Aidha Kamatri inasisitiza kuwa suala la upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama ni muhimu katika maeneo ya kambi zote.
3. Kamati ilielezwa kuwa baadhi ya taasisi za Serikali zinadaiwa na Idara hivyo Kamati inaagiza kuwa madeni hayo yalipwe na Idara ifanye juhudi za ziada kuyafuatilia madeni hayo.
4. Kamati minjaiomba Wizara kuwa inaiombe kambi ya Chuoc ha Mafunzo Wete fedha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo yhao au iingizwe katika bajeti kuu ya Serikali kwaa kuingizwa katika eneo la miradi ya maendeleo.
5. Kamati inaishuri Idara ya Chuo cha Mafunzo iwaendeleze wanasheria wake kwa kuwapeleka katika katika ofisi za Mkurugenzi wa Mashtaka kwa lengo wa kuwapiga msasa na kuwafanya wawew makini zaidi katika utekelezaji wa majukumu yao.
6. Kamati inaishauri Serikali inapoandaa bajeti pam,oja nba mambo mengine iangalie na vipaumbele na unyeti uliopo katika ofisi mbali mbali pamoja na mahitaji yaliyopo.
7. Pamoja na changamoto nyingi zilizopo katia Idara ya Chuo cha Mafunzo kisiwani Pemba, Kamati inapenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Idara kwa upoande wa Pemba kutoaka na juhudi mbali mbali walizozichukua ikiwemo kuuza weneo lao kwa ajili ya kupata fedha za kuedneshea shughuli zao za kimaendeleo ikiwemo kujenga

gereza jipya katika Kambi ya Kengeja ambapo gereza hilo limeanguka kutokana na upepo.

8. Wakati wa ziara yake katika kambi mbali mbali ya Idara hii, Kamatimilipewa taarifa kuwa suala la uhamisho kwa baadhi ya watumishi limekuwa ni tatizo sugu kutokana na nbaadhi ya wakubwa kuwakingia kifua baadhi ya watumishi wasipelkwe kisiwani Pemba jambo ambalo limkuwa nim kero kubwa kwa baadhi ya watumishi ambao muda wao wa kurudi Unguja unakuwa umefikia lakini mkutokana na halki hiyo hawarudishwi, hivyo Kamati inaishauri Wizara kuliangalia tatizo hilo kwa kina na kuwahamisha watu7mishi kwa mujibu wa Utaratibu wa kisheria uliopo na sio kusikiliza wakubwa wanasema nini.

ZIARA YA KAMATI YA KUJIFUNZA KATIKA MAGEREZA YA SEGEREA NA UKONGA DAR ES SALAAM

Kamati katika kujifunza shughuli za uendeshaji Taasisi zinazosiamia sheria, haki za binaadamu na utawala ilitembelea magereza ya Segerea na Ukonga, Dar es Salaam, mnamo tarehe 4/01/2015 kwa lengo la kuona na baadaye kuishauri Serikali kupitia Chuo cha Mafunzo kutekeleza mambo mbali mbali ambayo kamati imeyabaini katika ziara hiyo kama ifuatavyo:-

1. Kamati ilipata nafasi ya kujifunza namna ya upatikanaji wa huduma ya vyukula vya msingi ikiwemo chakula maalumu kwa wagonjwa na huduma ya kwanza ya afya kwa wafungwa.
2. Pia, Kamati ilijionea jinsi kazi za amali za urekebishaji tabia zimeimarishwa, wafungwa wanafunzwa kazi za uzalishaji kama kuchonga, kushona, uashi, ufumaji na kazi mbali mbali za amali.
3. Kamati ilijifunza jinsi Magereza wanavyozilinda haki za wafungwa kupata huduma za sheria na kiroho.
4. Kamati pia ilipata nafasi ya kujua haki za wafungwa kupata habari, elimu na mengineyo. Aidha, Kamati ilikuta darasa la kusomeshwa wafungwa, mahabusu na watoto ambapo ilipata taarifa za wafungwa wanaoendelea na masomo yao ya juu wakiwa gerezani.
5. Vile vile Kamati ilielezwa jinsi mabadiliko ya uendeshaji Magereza kupitia Sera na Sheria.
6. Kamati ilijionea jinsi jeshi la Magereza lilivyojiimarisha kwa kuweka miundombinu ya mizuri na logistiki ambapo Magereza wanapeleka mahabusu Mahakamani kwa vyombo vyao wenyewe.
7. Kamati pia ilijionea hali ya usafi wa hali ya juu katika mahabusu hasa ya wanawake.
8. Paia Kamati iliona jinsi jeshi la Magereza lilivyoweza kutenganisha mahabusu ya watoto na watu wazima. Aidha magereza wamegawanya maeneo ya wafungwa kama vile eneo la Bush limewekwa kwa wafungwa wenye vifungo vifupi na wenye tabia njema, eneo la ‘tailor wing’ wanakaa wafungwa wenye vifungo virefu na wafungwa hatari, eneo la ‘condemn’ wanalokaa wafungwa wa kunyongwa, eneo maalumu la mahabusu wanalokaa mahabusu na watu hatari na eneo la wafungwa na mahabusu wa uharamia.

9. Wafanyakazi wa magereza kuwekewa utaratibu wa kupata unafuu wa huduma za lazima ‘duty free shop’.

MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA SERIKALI KUPITIA CHUO CHA MAFUNZO KUTOKANA NA ZIARA HIYO :-

1. Kamati inaishauri Serikali kuimarisha huduma za chakula na za awali za afya kwa wanafunzi.
2. Kamati inahsauri kazi za amali au mafunzo ziimarishwe ili wanafunzi wakimalizia vifungo vyao wawe na ujuzi maalumu kwa lengo la kuwasaidia kuendesha maisha yao.
3. Pia Kamati inashauri kuimarishwa kwa haki za binaadamu za wanafunzi na mahabusu kama vile elimu, habari ne nyenginezo.
4. Kamati inashauri kuwekwa mazingira safi kwa ajili ya afya za wanafunzi na wafanyakazi.
5. Kamati inashauri kuimarishwa kwa miundombinu ya magereza na logistiki.
6. Kamati inashauri mahabusu za watoto na watu wazima ziwekwe tofauti na watoto wapatiwe huduma maalumu ya ushauri wa akili ‘psychiatric’.
7. Kamati inazidi kuisisitiza na kuishauri Serikali kuimarisha maslahi ya wafanyakazi wa Vyuo vya Mafunzo kama vile kupatiwa huduma zote za msingi na mahitaji ya lazima kwa bei nafuu ‘duty free shops’

KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI (KZU)

Kikosi cha Zimamoto na uokozi ni miongoni mwa Idara Maalum za SMZ ambacho kina jukumu la ulinzi pamoja na kukioa maisha yan wat una mali zao na kutoa hudum,a kwa jamii pamoja na elimu kwa ajili ya kujikinga nba majanga ya aina mbali mbali.

Kamati ilifanya ziara ya kukagua katika kambi mbali mbali za Idara hii ambapo huko mkisiwani Pemba kamati ilikagua kambi ya Mkoani na kujiona shughuli zinazofanbywa na kikosi hiki. Katika ziara hiyo, kamati ilipokea tarifa ya utekelezaji wa shuguli za Idara na kukutana na chqangamoto mbali mbali zinazoikabili Idara hii.

CHANGAMOTO ZA KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI

Kamati ilipewa tarifa ya changamoto zifuatazo:

1. Ukosefu wa majengo ya ofisi na sehemu za kulala askari. Katika ziara hiyo, Kamati ilishuhudia hali mbaya ya maeneo ya Ofisi katika kambi ya Mkoani ambapo Kamati ililazimikam kusimama nje kwa ajili ya kupokea tarifa ya utekelezaji wabajeti. Aidha Kamati ilisikitishwa sana na hali hiyo pamoja na kukumbana na suala la ukosefu wa maeneo ya makaazi ya askari ambapo Kamati iliwashuhudia askari hao wote wakikusanyika katuika bweni moja na kufanya shughuli zao zote humo humo ikiwemo malazi, makazi nakadhalika. Aidha Kamati ilielezwa kuwa baadhi ya askari hao wengine wanaishi kwa jamaa zao na wengine wanaishi katika nyumba za kupanga katika maeneo tofauti ambapo ***“House allowance”*** hawapatiwi.
2. Aidha Kamati ilielezwa kuwa Kikosi cha Zimamoto kinakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa vifaa vya uhakika ambapo vifaa vilivyopo kwas asa havikidhi haja kutokana na uchakavu wa vifaa hivyo na kusababisha malalamiko mbali mbali kutoka kwa wananchi.

3. Kutoshirikishwa kikamilifu katika uandaaji wa bajeti ya Idara pamoja na kutojua kiwango halisi cha fedha zilizotengwa kwa upande wa Pemba ni miongoni mwa changamoto kubwa zinlizopo.
4. Aidha Kamati ilielezwa kuwa kituo cha Mkoani hakina eneo la parking kwa ajili ya kuweka gari zinazotumika kwa ajili ya kazi za kuzima moto.
5. Kamati pia ilielezwa kuwa Kikosi cha Zimamoto katika eneo la Mkoani na Wete hawana eneo lao na wanatumia maeneo ya kuazima ambapo kwa upoande wa Wete wanatumia eneo la Wizara ya Kilimo na kwa upande wa Mkoani wanatumia eneo la Shirika la Banadari. Aidha Kamati ilielezwa kuwa kwa upande wa Mkoani eneo hilo wanalolitumia halitoshi kwa matumizi yao kutokana na shughuli zao za kila siku.Hata hivyo, Kamati ilielezwa kuwa kwa upande wa Wete Kikosi cha Zimamoto kimepatiwa eneo kwa ajili ya kujenga ofisi zao lakini kutokana na ukosefu wa fedha wanashindwa kujenga kituo hicho.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kujenga Afisi za Zimamoto kwa Wilaya zote za Pemba. Aidha Kamati inashauri kwa upande wa Wete na Mkoani ni vizuri vituo hivyo vikajengwa katika maeneo ya bandari kutokana na unyeti wa maeneo hayo hasa zinapotokezea ajali za baharini ambapo itakuwa ni rahisi kwa askari waliopo vituoni humo kufika haraka katika eneo la tukio.
2. Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha kuwa gari zinazotumika katika shughuli za uokozi zinakidhi haja na kuhakikishia kuwa inafanya juhudi za makusudi kukiksaidia Kikosi cha Zimamoto na uokozi kupata maji ya uhakika kwa ajili ya kutekeleza shughuli zake kwa uhakika.
3. Kamati inaagiza kushirikishwa kwa vituo vyote katika suala zima la uandaaji wa Bajeti kutokana na baadhi ya vituo hasa vilivyopo kisiwani Pemba kukosa fedha za kuendeshea shughuli zake zilizopangwa na kusababisha shughuli hizo hizo kujirudia katika bajeti inayofuata.
4. Kamati inaagiza kuangaliwa upya suala la kuawalipa wafanyakazi posho zao za malipo ya nyumba hasa kutokana na baadhi ya watendaji kukosa maeneo ya kuishi na kulazimika kukodi maeneo yaliyo nje na kambi na kulipa kodi ambapo kodi hizo hulipiwa kwa fedha zao wenyewe, hivyo Kamati inaishauri Wizara kuliangalia upya suala hilo hasa kutokana na hali halisi ya maisha ilivyo hivi sasa ambapo maisha yamezidi kuwa magumu na kusababisha hali za askari kuzidi kuwa ngumu.
5. Kamati inaushauri Wizara kufanya juhudi za makusudi za kukipatia kikosi cha Zimamoto vitendea kazi vitakavyokidhi haja katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

KIKOSI CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM)

Kikosi cha Kuzuia Magendo kina jukumu la kuhakikisha kuwa kinazuia usafirishaji wa mali yoyote ambayo imezuiwa kisheria kusafirishwa katika maeneo mbali mbali ya ndani na nje ya mipaka ya nchi yetu.

Katika kuhakikisha kuwa utekelezaji wa shughuli hiyo unafanyika kwa ufanisi Kamati ya Katiba, Sheria na Utawaqla ya Baraza la Wawakilishi katika ziara zake za kawaida ilikagua maeneo mbali mbali ya Kikosi hiki na kushuhudia utekelkezaji kwa baadhi ya ameneo na kukutana na changamoto mbali mbali ambazo zimekuwa ni kikwazo kwa utekelezaji wa majukumu ya idara kwa baadhi ya meneo.

CHANGAMOTO ZA KIKOSI CHA KUZUIA MAGENDO

1. Kamati ilielezwa kuwa Kikosi cha Kuzuia Magendo kinakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti jambo ambalo hupelekea mipango mingi kuishia kwenye maandishi na kutotekelezwa kwa muda uliopangwa. Aidha Kamati ilielezwa kuwa Kikosi cha Kuzuia Magendo hasa kwa upande wa Pemba kina mpango madhubuti wa ujenzi wa vituo vya afya lakini changamoto kubwa ilikuwepo ni ukosefu wa fedha.
2. Pia kuna changamoto ya wingi wa bandari bubu hasa kwa upande wa kisiwa cha Pemba jambo ambalo limekuwa ni changamoto kubwa kutokana wingi wa matukio hayo ya magendo na hasa ikrikali izingatiwa changamoto ya vitendea kazi inayowakabili wapiganaji wa kikosi hicho.
3. Kamati ilipofanya ziara katika kambi ya Makombeni ilielezwa kuwa eneo hilo linamilikiwa na wananchi jambo ambalo limekuwa ni changamoto kutokana na unyeti wa shughuli kiaskari.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaiahsauri Wizara kusaidia upatikanaji wa hati miliki katika baadhi ya maeneo yanayotumiwa na Kikosi cha Kuzuia magendo na inaiomba Serikali kufanya utaratibu wa kuwalipa fuidia wananchi wenye umiliki wa maeneo hayo na hatimaye kikosi hicho kiweze kuyamiliki maeneo hayo na kiweze kuyatumia kwa shughuli zao za kila siku kwa utulivu.
2. Kamati inazidi kuisistiza Serikali kutoa bajeti ya kutosha kwa vikosi maalum hasa kwa upande wa Pemba kutokana na shughuli za vikosi hivyo kukwama kutokana na ukosefu wa bajeti ya kutosha
3. Kamati inaishauri Wizara kulifuatilia la ujenzi wa afisi ya uokozi katika eneo la Bandari ya Mkoani kutokana na umuhimu wa kituo hicho ambapo mpaka sasa hivi Shirika la Bandari Mkoani bado halijatoa majibu yoyote kuhusiana na jambo hilo. Hta hivyo, Uongozi wa KMKM ulitoa taarifa kwa Shirika la Bandari kuwa wako tayari kuanza ujenzi wakati wowote watakapo ruhusiwa, hivyo kamati inaiomba Wizarea kulifuatilia jambo hilo ili ujenzi huo uweze kuanza mara moja.

JESHI LA KUJENGA UCHUMI (JKU)

ZIARA YA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA YA BARAZA LA WAWAKILISHI DAR ES SAALAAM KUANZIA TAREHE 2/01/2015 MPAKA 5/01/2015.

Lengo la ziara lilikuwa ni kujifunza shughuli mbali mbali za JKT ambazo Kamati ilijifunza na hatimae kuja kuishauri Serikali kuwezesha shughuli kama hizo kufanywa na JKU kwa lengo la kujenga uchumi kama malengo ya kuanzishwa kwake yalivyo:-

KATIKA ZIARA HIYO KAMATI ILIJIFUNZA YAFUATAYO:-

1. Malezi ya vijana, dhana ya kuwajenga kujitegemea na kuepuka utegemezi.
   Kamati imeona shughuli wanazofundishwa vijana ambazo stadi za kazi kama kilimo, ufugaji bora, uvuvi, useremala, uashi, ufundi magari na mitambo, ufundi umeme, ushonaji na mengineyo. Shughuli hizi zote vijana hufundishwa na wakimaliza wanaweza kujitegemea.

2. **Ubunifu wa Kitaasisi katika kuzalisha mali.**

Kamati imeona miradi mingi ya JKT inawapa fursa ya kubuni miradi mengine ya uzalishaji kwa mfano, katika mradi wa kuingizwa matrekta JKT ilitumia kampuni binafsi kufanya utoaji na usafirishaji wa matrekta hayo, baadaye walibuni kampuni yao wenyewe ya utoaji na usafirishaji (clearing and forwarding).

3. **Kutumika wataalamu wa fani mbalimbali ipasavyo katika uzalishaji mali.**
   Katika kuendeleza shughuli za uzalishaji, JKT imewekeza katika kupata wataalamu wa fani mbali mbali katika kiwango cha shahada na zaidi. Kamati imekuta miradi mingi inaendeshwa na wataalamu wenye elimu za juu katika fani za uchumi, biashara, sheria, uongozi nakadhalika.

4. **Uzalishaji mali wenye malengo ya kupata faida.**
   JKT imekuwa na miradi ya Ujenzi mfano jengo kubwa la Msasani Complex Center limejengwa na kampuni ya ujenzi ya JKT na hivi sasa JKT inaendesha miradi mipya ya ujenzi ikiwemo ujenzi wa Hospitali ya matibabu ya ugojwa wa Ebola awamu ya kwanza wenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni 200. Miradi mengine ni ya viwanda, utalii, matrekta, huduma za ulinzi na 'clearing and fowarding'.
5. **Utambuzi kushughulikia miradi na uwekaji mzuri wa mapato**
   Kamati imejifunza miradi yote ya JKT inatambuliwa na uendeshaji wake pamoja na gharama, hasara na faida vinafanyiwa tathmini kila muda.

6. **Uwepo wa Soko la bidhaa na huduma zinazozalishwa JKT**
   Kamati imeona JKT inajitangaza na kutangaza bidhaa na huduma inazotoa ambazo zimeweza kutoa ushindani na kampuni nyengine, aidha taasisi za Serikali zimekuwa ni wanunuzi wa bidhaa na huduma za JKT.

7. **Jitihada za SMT katika kusaidia hali na mali JKT kutekeleza malengo yake.**
   Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa inaiamini JKT kwa kuiwezesha na kuipa miradi mikubwa ambayo wanaimudu, kwa mfano JKT wamepewa na Serikali mradi wa matrekta ambao umetokanana mkopo nafuu kutoka kwa Serikaili ya India, kiasi cha dola za kimarekani milioni 40 zimewekezwa.

8. **Sheria nzuri inawezesha JKT kuongeza wigo mpana wa uzalishaji kwa kuunda taasisi tanzu za uzalishaji mali.**
   Ktokana na uwepo wa sheria nzuri ya Mashirika ya Umma namba 23 ya mwaka 1974 (Corporate Sole Establishment Act No.23 of 1974), ambayo inawezesha taasisi ya Serikali kuanzisha shirika la kibiashara, sheria hiyo ndiyo iliyotumiwa na JKT kuanzisha Shirika la Uzalishaji Mali la JKT (SUMA JKT) pamoja na amri ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1982. Kwa sheria hiyo SUMA JKT imeweza kuanzisha kampuni zake tanzu nyengine kama SUMA JKT Guard Ltd na Kampuni ya Ujenzi ya National Service Construction Department.

9. **Nidhamu ya viongozi na watendaji katika kusimamia kazi na uzalishaji mali ni za hali ya juu (JKT Ruvu).**
   Kamati imetembelea KJ 832 Mlandizi ambapo jambo kubwa ambalo Kamati imejifunza ni mafanikio ya uzalishaji mali yaliyotokana na uongozi makini wenye kusimamia

majukumu yake kwa nidhamu, Kamati imeona kuwa Mkuu wa Kikosi cha JKT Mlandizi anatambua shughuli zote za uzalishaji mali kwa undani na kila shughuli anaifuatilia yeye mwenye binafsi, hali ambayo imewafanya wasaidizi wake wote wafanyekazi kwa mtazamo wake wa kiuongozi wa kuwajibika na kujituma. Kamati imejifunza kuwa hili ni jambo kubwa katika kushawishi mabadiliko na ufanisi katika kazi ambazo JKU wanalazimika kuzifanya.

MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA SERIKALI KUPITIA JKT KUTOKANA NA MAFUNZO YA ZIARA HIYO:-

1. Kamati inaishauri Serikali ihakikishe kuwa malezi ya vijana yahakikishe kuwa yanawajengea uwezo wahitimu ambao utawawezesha kujitegemea na kuweza kuzalisha mali kwa nguvu zao wenyewe. Kamati inashauri Serikali, ili JKU iweze kufikia malengo yake lazima mtazamo wa malezi ya vijana ubadilike, uwe wenye kuwezesha vijana kupata ustadi za kweli badala ya vijana kutegemea ajira za Serikalini pekee hata baada ya kuhitimu mafunzo yao.

2. Rasilimali zilizopo zitumike kubuni miradi mengine ya uzalishaji mali yenye faida. Kamati inashauri JKU kufanya tathmini ya fursa zilizopo za rasilimali ya ardhi, bahari na utalii na kubuni shughuli makini za uzalishaji, JKT wamepata fursa kama hizo na wameweza kubuni shughuli nyingi za uzalishaji mali.

3. Kamati inaishauri Serikali kuajiri wataalamu katika fani mbali mbali za uzalishaji mali. Mtazamo wa ajira katika jeshi ubadilike, pamoja na kuwa JKU na idara nyengine maalumu huajiri wafanyakazi katika ngazi za chini za elimu lakini sasa mtazamo huo ubadilike kwa kulifanya jeshi liwe na wataalamu wa elimu za juu kama wenzetu wa JKT, hali hiyo itawafanya vijana wetu wathamini elimu kwa kuwa fursa za kazi za elimu ya kiwango kidogo zitakuwa hazipo.

4. Kamati inalishauri Jeshi la Kujenga Uchumi kujiwekea malengo ya kupata faida na mitaji ya uzalishaji. Ili maendeleo endelevu ya JKU yaweze kupatikana ni vyema jeshi hilo likajiwekea malengo ya kila mwaka kwa kila mradi wanaoufanya na wakikishe kuwa mradi huo unaleta faida kwa kiasi kikubwa kama wenzetu wa JKT wanavyofanya.

5. Kamati inashauri miradi ya JKU itambuliwe na kufanyiwa uchambuzi wa nguvu za uzalishaji, udhaifu na fursa ya kuiendeleza. Aidha Kamati inapendekeza uchambuzi wa shughuli za uzalishaji mali ufanyike kama zinaleta faida kwa JKU na kama faida hiyo inaelekea kuifanya JKU kuwa chombo cha kujenga uchumi wa nchi kama lengo la kuundwa kwake lilivyo.

6. Kamati inaishauri Serikali ihamasishe taasisi za Serikali kutumia huduma na bidhaa zinazozalishwa na JKU (fanicha na huduma ya ulinzi na nyenginezo). Kamati inaishauri Serikali kama vile ilivyohamasisha wafanyakazi wa Serikali kupokelea mishahara yao Benki ya PBZ na kusaidia benki hiyo kumudu ushindani na benki nyengine, inawezekana pia ikazihamasisha taasisi nyengine za Serikali kununua fanicha na kupata huduma nyengine za ulinzi kupitia JKU badala ya kuagizia kutoka nje ya nchi au kwa wafanyabiashara binafsi na kuitia gharama kubwa Serikali.

7. Kamati inaishauri Serikali isaidie JKU kwa kuipatia mitaji na miradi ili ijiongezee uwezo na kipato (miradi ya uchongaji vikalio, nguo n.k) JKT waliishauri Kamati iishauri Serikali kuisaidia JKU kwani bila ya msaada wa Serikali haiwezi kufikia hatua kubwa kama JKT.

8. Kamati inashauri mabadiliko ya sheria yafanyike ili yawezeshe JKU na Idara nyengine maalumu kuongeza wigo mpana wa uzalishaji mali. Sheria zetu bado hazijawa wazi kwa taasisi za Serikali kuweza kuanzisha vyombo vya uzalishaji mali kama Mashirika au Kampuni, bado ipo dhana ambayo siyo shahihi sana inavyotumika ya kuwa Serikali haifanyi biashara wakati Serikali nyingi bado zimejibakisha katika biashara za huduma ambazo sekta binafsi inaposhindwa Serikali inakuwa karibu kuokoa huduma ziendelee kwa wananchi wake.

9. Kamati inashauri uongozi wa JKU uhakikishe nidhamu ya hali ya juu inawekwa kwa viongozi na askari ambao watafanikisha juhudi za uzalishaji mali kama ilivyo kwa JKT.

MAONI NA MAAGIZO YA JUMLA YA KAMATI KWA TAWALA ZA ` MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

1. Kamati inazishauri mamlaka za Serikali za mitaa zihakikishe kuwa zinaajiri wataalamu wa fani mbali mbali ili kuimarisha utendaji kazi katika kila ngazi .
2. Kamati inaagiza matakwa ya sheria mpya ya Serikali za mitaa na Tawala za Mikoa yatekelezwe kwa kila Serikali ya Mtaa kusimamia majukumu yake katika kila eneo lake inavyopasa.

3. Kamati inaagiza Serikali za Mitaa kuwapa elimu watendaji wake, wakiwamo masheha na madiwani na watendaji wengine kuhusu masharti ya sheria mpya za Tawala za Mikoa na sheria ya Serikali za Mitaa.

4. Kamati inashauri Serikali za Mitaa kuhakikisha zinafikia malengo ya ukusanyaji mapato katika maeneo yao na kuhakikisha mapato hayo hayavuji.

5. Kamati inashauri huduma za jamii katika maeneo ya Serikali za Mitaa zisimamiwe ipasavyo na migogoro mbali mbali ya kimipaka na ardhi itafutiwe ufumbuzi kwa mujibu wa sheria kabla ya kufika katika vyombo vyengine.

6. Kamati inaagiza Serikali za mitaa zisimamie hali ya usalama na amani katika maeneo yao na kuhakikisha kuwa ishara zozote za matendo ya uvunjifu wa amani, udhalilishaji wa kijinsia, uharibifu wa mazingira na matendo mengineyo yanachukuliwa hatua haraka kwa mujibu wa sheria.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

Wizara ya Katiba na Sheria inaundwa na Idara zifuatazo:

1. IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI.
2. IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI.

3. MAHAKAMA.
4. AFISI YA MWANASHERIA MKUU ZANZIBAR.
5. TUME YA KUREKEBISHA SHERIA.
6. AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA.
7. AFISI YA MUFTI WA ZANZIBAR.
8. WAKALA WA USAJILI BIASHARA NA MALI.
9. AFISI YA MRAJISI WA VIZAZI NA VIFO.
10. AFISI YA MSAJILI WA HAKIMILIKI.
11. KMAISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA.

MAHAKAMA

Mahakama ni miongoni mwa mihimili mikuu ya Serikali ambapo ina haki na wajibu wa kuhakikisha kuwa haki za raia zinalindwa na haki hiyo inatendeka kwa kuzingatia sheria zilizopo.
Kamati katika ziara ya kikazi iliyoifanya katika muhimili huu ilipokea taarifa ya utekelezaji wa bajeti pamoja na kupokea changamoto mbali mbali zilizopo katika taasisi hiyo.

CHANGAMOTO

1. Kamati ilielezwa kuwa kuna changamoto ya mishahara ya Mahakimu wa mahakama za mwanzo ambapo mishahara yao bado ni midogo ukilinganisha na Mahakimu wengine.
2. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa uhaba wa fedha unazorotesha ukarabati wa Mahakama za Unguja na Pemba.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

3. Kamati inashauri utaratibu wa kuangalia malipo ya Mahakimu wa Mahakama za mwanzo ubadilike kwa kuwa Mahakimu wanaweza kulipwa kwa hadhi zao badala ya viwango vya elimu, mafano mtu akiwa Mbunge bila kujali ana elimu gani analipwa kulingana na hadhi ya nafasi hiyo, utaratibu huo unaweza kufanyika kwa Mahakimu ambao mtu akiwa hakimu wa ngazi fulani basi alipwe kulingana na ngazi hiyo.
4. Kamati inashauri fedha za kuendeleza ujenzi na ukarabati wa Mahakama zipatikane ili ukarabati huo uendelee mfano ukarabati wa jengo la Mahakama ya Chake Chake unakwenda taratibau kutokana na ukosefu wa fedha.

AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA

Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ina jukumu la kusimamia mashtaka na kufungua kesi katika Mahakama kwa lengo la kuhakikisha kuwa haki inatendeka.
Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi ilifanya ziara katika Afisi hii Unguja na Pemba na kupekea taarifa ya utekelezaji wa bajeti pamoja na kukagua miradi mbali mbali inayosimamiwa na Afisi hii. Kwa ujumla Kamati iliridishwa na kiwango cha miradi inayosimamiwa na Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kilipofikiwa kutokana na hali ya miradi hiyi kuwa katika hatua ya

kuridhisha. Hata hivyo Kamati ilielezwa changamoto mbali mbali zilizopo katika Afisi hiyo.

CHANGAMOTO ZA AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA

1. Kamati ilielezwa kuwa Afisi ya Mkurugenzi wa mashtakata inakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti na majukumu ya kazi ni mengi ambayo yanaathiriwa na bajeti ndogo na hiyo inayokasimiwa haitolewi kwa kutosheleza, aidha bajeti ya Ofisi ya DPP ni ndogo ukilinganisha na taasis nyengine za Serikali ambazo zina majukumu madogo lakini bajeti zao ni kubwa.
2. Kamati pia ilielezwa changamoto ya ukosefu wa ushirikiano kutoka kwa wananchi kwa lengo ala kutoa ushahidi bado ni mdogo sana jambo ambalo ni changamoto kubwa katika uendeshaji wa kesi.
3. Kamati ilielezwa kuwa waendesha mashtaka wanakabiliwa na tatizo sugu la maslahi duni pamoja na wasaidizi wao licha ya kazi ngumu wanayoifanya. Aidha, Kamati pia ilielezwa kuwa suala la usalama wa waendesha mashtaka kuwa mdogo ni changamoto kubwa na hasa ikizingatiwa kuwa wanafanya kazi za kujitoa muhanga. Kutokana na hali hiyo, wanasheria wengi wa Afisi ya Mkurugenzi wa mashtaka wanakimbilia katika fani ya uendeshaji wa mashtaka pamoja na fani nyengine kwa lengo la kupata maslahi mazuri yatayoweza kuwasaidia na familia zao.
4. Vile vile, changamoto ya ukosefu wa jengo la ofisi na maktaba yenye vitabu vya kutosha vya sheria na vyengine kwa ajili ya rejea za kesi mbali mbali ni changamoto kubwa inayoikabili ofisi hii hasa kisiwani Pemba.
5. Changamto nyengine kubwa ambayo hadi sasa ufumbuzi wake haujapatikana ni suala la uelewa mdogo wa baadhi ya wadau na wananchi kwa ujumla kuhusiana na suala zima la usimamizi wa haki katika mashauri ya jinai hususan katika suala la dhamana na wadhamini. Pia kutopatikana kwa suluhisho muafaka kwa kesi za udhalilishaji wa wanawake na watoto kutokana na kukosekana kwa kipimo cha DNA ni changamoto kubwa sana ambayo ufumbuzi wake bado haujapatikana.
6. Kamati ilielezwa kuwa Afisi hasa kisiwani Pemba inakabiliwa na suala la ukosefu wa wataalamu kutoka taasisi nyengine ambazo zinashirikiana na Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka hasa katika fani ya uchunguzi wa maiti (Pathologist) ni changamoto kubwa hasa ikizingatiwa kuwa suala hilo lipo kwa mujibu wa sheria.
7. Aidha Kamati ilielezwa kuwa Afisi ina ukosefu wa usafiri kwa Unguja na Pemba na suala la ukosefu wa makaazi kwa watendaji wa kisiwa cha Pemba ni suala linalopelekea baadhi ya shughuli za ofisi kukwama. Kamati ilielezwa kuwa ofisi ina gari mbili kisiwani Pemba lakini zote mbovu jambo ambalo limekuwa ni kero kubwa kwa watendaji wa ofisi hii.
8. Aidha Kamati ilipatiwa taarifa kuwa ofisi haina mlinzi jambo ambalo ni hatari kubwa kwa usalama wa ofisi na hasa ikizingatiwa nyaraka mbali mbali muhimu zilizokuwemo ndani.
9. Kamati pia iliwelezwa kuwa Afisi inakabiliwa na changamoto ya kutokulipwa kwa mashahidi jambo ambalo hupelekea aidha kuchelewa sana kwa kesi kumalizika au kufutwa moja kwa moja.
10. Changamoto nyengine iliyoko hasa kisiwani Pemba ni suala la Wanasheria wa Chuo Cha Mafunzo kukosa elimu ya smingi ya "*Drafting"* jambo ambalo

hupelekea wanapoandaa *"Appeal au Judgement"* kukataliwa katiaka Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na kusababisha mrundikano mkubwa wa mahabusu.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuongeza maslahi ya waendesha mashtaka kutokana na kazi nzito na ngumu wanayoifanya na amabyo inahatarisha uhai wa maisha yao. Aidha, Kamati inasisitiza kuwa pamoja na mipango mingi ya Serikali iliyopo, ni vyema kukawekwa vipaumbele katika kila sekta na kuangalia umuhimu ili kuwatia moyo watendaji wanaofanya kazi katika mazingira hatarishi. Aidha Kamati kisiwani Pemba ilipewa taarifa kuwa msaidizi wa Mkurugenzi wa Mashtaka kisiwani Pemba anatakiwa alingane na Naibu DPP kimaslahi suala ambalo halipo kwa hivi sasa, hivyo Kamati inasisitiza suala hilo kuangaliwa upya.
2. Kamati imesikitishwa na taarifa iliyopatiwa kuwa kisiwani Pemba tatizo la mtaalamu wa kuchunguza maiti (Pathologist) na kupelekea ushahidi kukosekana, hivyo Kamati inaishauri Serikali kulishughulikia tatizo hilo ili haki iweze kutendeka pamoja na kuongeza idadi ya wakemia watakaosaidia kurahisisha kazi za waen desha mashtaka.
3. Kamati inazidi kuisisitiza Serikali kulichukulia hatua suala la upatikanaji wa kipimo cha DNA ili kesi za udhalilishaji wa wanawake na watoto ziweze kupungua. Hali hii inatokana na idadi kubwa ya kesi zinakosa ushahidi kutokana na kukosekana kwa kipimo hicho ambapo kisiwani Pemba Kamati ilielezwa kuwa kuna kesi tokea mwaka 2006 imekosa ushahidi DNA na mpaka leo sample yake haijarudi, hili ni suala la kusikitisha na kuwakatisha tama wananchi.
4. Pamoja na hali duni ya upatikanaji wa fedha, Kamati inaisistiza Afisi ya Mkurugenzi wa mashtaka kuzidisha juhudi zake kwa kuwatafutia maeneo ya kusihi watendaji wake huko kisiwani Pemba pamoja na usafiri wa uhakika kwa ajili ya ofisi.
5. Suala la ofisi za kudumu ni muhimu sana kwa ofisi pamoja na kuongeza vitabu kwa ajili ya rejea za kesi, hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuitafutia Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ofisi ya kudumu ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi. Aidha Kamati inaagiza kutafutwa kwa vitabu vya rejea kwa ajili ya waendesha mashtaka wa Pemba.
6. Kamatgi inatoa agizo la kulipwa kwa mashahidi wote wanaoshiriki katika kutoa ushahidi wa kesi mbali mbali ili kesi hzio ziweze kuendelea na haki kutendeka kwa watu wote.
7. Kamati inaiagiza Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kushauriana na hatimaye kukubaliana kwa gharama nafuu na Idara ya Chuo cha Mafunzo ili Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka iweze kutoa mafunzo ya msingi ya *"Drafting"* kwa wanasheria wa Chuo cha Mafunzo kwa lengo la kuondoa tatizo lililopo la mrundikano wa mahabusu uliopo hivi sasa.
8. Kamati imesikitishwa na suala la ukosefu wa mlinzi wa kudumu katika Afisi ya Mkurugenzi wa Mahstaka Pemba na hivyo inatoa agizo la kuajiriwa kwa mlinzi kwa ajili ya kulinda usalama wa Afisi.
9. Kamati inazidi kuisisitiza Serikali kuipatia vyombo vya usafiri Afisi ya DPP kwani tokea ilipopatiwa gari mbili za msaada na UNDP kwa hapa Unguja, ambazo zimeshachakaa na hazitoshi tena kutokan n a kuongezeka kwa majukumu

ya Afisi, imekuwa inaleta usumbufu kwa Afisi ya DPP kushindwa kufatilia na kusimamia uendeshaji wa Mashitaka katika maeneo mengine yanayoendesha kesi za jina na jeshi la Polisi.

10. Kamati inaishauri Serikali kuongeza bajeti kwa Afisi ya DPP ili iweze kutoa elimu kubwa kwa wananchi weweze kuhamasika kutoa ushahidi kwani hakuna hatia bila ya ushahidi.

WAKALA WA USAJILI BIASHARA NA MALI

Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali ni taasisi yen ye majukumu ya kusimamia masuala ya usajili yanayohusu taasisi za biashara, hati za mali ubunifu, pamoja na usajili wa nyaraka mbali mbali zinazowahusu wananchi na wageni wanaofanya shughuli zao Zanzibar.

Katika kipindi cha kazi za Kamati, Kamati ilipata nafasi ya kufanya ziara kisiwani Pemba ambapo ilielezwa kuwa taasisi inaendelea na kazi zake za kusimamia usajili na utunzaji wa nyaraka. Hata hivyo, Kamati ilielezwa changamoto kadhaa zilizopo katika taasisi hii.

CHANGAMOTO ZA WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA MALI

1. Kamati ilielezwa kuwa ofisi ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali bado haijatenganishwa na ofisi ya vizazi na vifo kisiwani Pemba kama ilivyuo Unguja.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaiagiza Wizara kufanya juhudi za kuzitenganisha ofisi hizo kisiwani Pemba na iwe kama ilivyo Unguja ili ziweze kufanya kazi kwa umakini na ufanisi mkubwa.

AFISI YA MRAJISI WA VIZAZI NA VIFO

Afisi ya Mrajisi wa Vizazi na Vifo inajukumu la kusajili vizazi na vifo pamoja na kutunza kumbukumbu zinazotokana na usajili huo. Kmamati ilipofanya ziara kisiwani Pemba ilipokea taarifa ya utekelezaji wa bajeti na jinzi afisi inavyofanya shughuli zake za kila siku ambapo ilielezwa kuwa katika kipindi cha Julai- Septemba, Afisi ilisajili jumla ya vizazi 1,935, hata hivyo Kamati ilielezwa kuwa bado uelewa wa wananchi ni mdogo sana katika suala zima la usajili wa vifo.

CHANGAMOTO ZILIZOPO KATIKA AFISI YA MRAJISI WA VIZAZI NA VIFO.

Kamati ilielezwa changamoto zifuatazo:

1. Afisi inakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa eneo la ujenzi wa ofisi katika Wilaya ya Wete. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa Afisi wanayotumia ipo ndani ya jengo la Afisi ya Mkuu wa Wilaya ambapo hali ya eneo hilo ni mbaya sana na kufanyiwa ukarabati ni gharama kubwa.
2. Afisi kisiwani Pemba inakabiliwa na ufinyu wa bajeti hali inayopelekea kukosekana kwa magamba ya kutengenezea vyeti.
3. Aidha Kamati ilielezwa kuwa Afisi inakabiliwa na ukosefu wa vitendea kazi hasa usafiri ambapo kwa hivi sasa ksiwani Pemba ofisi ina honda moja, aidha Kamati ilielezwa kuwa ofisi hii haijawahi kupatiwa gari tokea mwaka 1993 jambo ambalo limekuwa likikwamisha baadhi ya shughuli muhimu za kiutendaji.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

Baada ya kupokea taarifa na kukagua miradi mbali, Kamati ilikuwa na maoni na maagizo yafuatayo:

1. Kamati inaiomba Serikali kufanya juhudi za kutafuta eneo kwa ajili ya ujenzi wa ofisi katika Wilaya ya Wete ili kuondoa usumbufu uliopo hivi sasa na kuepuka gharama mara mbili za kukarabati eneo ambalo liko katika hali mbaya.
2. Kamati inaishauri Wizara inapoandaa bajeti taasisi na Idara zote za kisiwa cha Pemba zishirishwe kikamilifu na fedha wanazopangiwa kuingiziwa ziingizwe zote kwa mujibu wa bajeti ili angalau kupunguza baadhi ya changamoto zilizopo, hali ya ufinyu wa bajeti imepelekea suala la ukosefu wa magamga ya kutengenezea vyeti liisababishie ofisi ya Mrajisi wa Vizazi na Vifo kisiwani Pemba deni kubwa ambalo litachukua muda mrefu kulipwa. Afisi ya Mrajisi wa Vizazi na Vifo kwa hivi sasa inadaiwa zaidi ya shilingi milioni 51 na Idara ya Upigaji Chapa.Hivyo Kamati inalisisitiza hilo ili kuepuka madeni yasiyokuwa na ulazima.
3. Kamati inaishauri Wizara kuisaidia Afisi kupata usafiri wa gari ili iweze kuendesha shughuli zake kwa ufanisi zaidi.
4. Kamati inaishauri Wizara iipatie fungu lake Afisi ya Mrajisi wa Vizazi na Vifo hasa kwa vile ni taasisi inayojitegemea ili kuzipunguza changamoto zilizopo hivi sasa.
5. Kamati inaiagiza Afisi ya Mrajisi wa Vizazi na Vifo kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kusajili wa talaka na vifo ili afisi iweze kunufaika na mapato yatakayoingia.

MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

Kamati inaishauri Wizara ya Katiba na sheria kuwapatia usafiri wa uhakika Afisi kuu Pemba kwani hivi sasa Wizara ina gari moja,Naibu Mufti ana gari mbili na Afisi nya Msajili wa Vizazi na Vifo ina Honda moja, hivyo ni vyema kufanya utaratibu wa kuwasaidia usafiri wa uhakika kwa ajili kutekeleza wajibu wao.

WIZARA YA NCHI (AR) KAZI NA UTUMISHI WA UMMA

Wizara Nchi (AR) Kazi na Utumishi wa Umma inaundwa na Idara na Taasisi zifuatazo:

1. IDARA YA MIPANGO SERA NA UTAFITI.
2. IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI.
3. IDARA YA MAFUNZO NA MAENDELEO.
4. IDARA YA MIPANGO YA RASILIMALI WATU.
5. IDARA YA MIUNDIO YA TAASISI, UTUMISHI NA MASLAHI YA WATUMISHI.
6. IDARA YA NYARAKA NA KUMBUKUMBU ZA TAIFA.
7. IDARA YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO.
8. IDARA YA AJIRA.

9. IDARA YA USALAMA NA AFYA KAZINI.
10. OFISI KUU PEMBA.
11. KAMISHENI YA KAZI.
12. KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA.
13. TUME YA UTUMISHI SERIKALINI.
14. CHUO CHA UTAWALA WA UMMA.

IDARA YA MIUNDIO YA TAASISI, UTUMISHI NA MASLAHI YA WATUMISHI

Idara ina jukumu la kuhakikisha kuwa inakagua na kuhakiki watumishi kwa Taasisi za Umma ili iweze kupata taarifa za watumishi na kuona kama wamepangwa katika vyeo na daraja zao stahiki kulingana na miundo ya Utumishi.
Kamati ilipokuwa katika majukumu yake ilipatra nafasi ya kufanya ziara kisiwani Pemba na kupewa taarifa kuwa idara inaendelea na majuku yake kama kawaida sisipokuwa iuna changamoto nyingi ambazo zinakwamisha utekelezaji wa majukumu hayo.

CHANGAMOTO ZA IDARA YA MIUNDO YA TAASISI NA MASLAHI YA WATUMISHI WA UMMA

Kamati katika ziara yake kisiwani Pemba ilielezwa changamoto zifuatazo za idara:

1. Idara haina bajeti yake jambo ambalo linaisababishia idara hiyo ukosefu wa fedha na kushindwa kutekeleza majukumu yao.
2. Pia Kamati ilielezwa kuwa Idara inakabiliwa na changamoto katika baadhi ya ofisi za Serikali kuvunja masharti na sheria za kazi kwa kutowapatia wafanyakazi barua za uthibitisho wa kazini.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaishauri Wiuzara kuhakikiha kuwa inaitengea Idara bajeti hasa kisiwani Pemba ili kuiwezesha Idara hiyo kutekeleza wajibuy wake ipasavyo kama inavyopangwa katika bajeti.
2. Kamati inatoa agiza kwa Idara kuzichukulia hatua za kisheria taasisi na idara zote zitakazokuwa zinavunja sheria kwa kutowapatia wafanyakazi barua za uthibitisho muda unapofika wa kuwapa barua hizo.

KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA

Kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 katika kifungu cha 116 na kifungu cha 17 cha Sheria ya Utumishi wa Umma, namba 2 ya mwaka 2011, Kamisheni ni chombo cha juu kabisa kwa Tume zote za Utumishi na Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma na Wakala wa Serikali, chenye mamlaka ya kusimamia na kuratibu mambo yote ya Utumishi wa Umma kwa Zanzibar.

CHANGAMOTO

1. Kamati ilielezwa kuwa Kamisheni inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa fedha zinazopatikana kutokana na uhalisia kuwa fedha zinazotolewa hazilingani na zile zilizotengwa katika bajeti.
2. Changamoto nyengine ni udogo wa jengo la Afisi za Kamisheni.
3. Aidha Kamati ilielezwa kuwa Kmisheni inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa watumishi wenye elimu na uzoefu mzuri kama vile maafisa utumishi, sheria, uchumi na watafiti.
4. Kamisheni haina Mchunguzi na Mkaguzi wa ndani wa hesabu, Afisa Manunuzi, Afisa Takwimu na Mtunza Ghala.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inashauri Serikali kuisaidia Kmisheni kutatua tatizo la upungufu wa watendaji katika nafasi mbali mbali.
2. Kamati inashauri Kamisheni ipatiwe nafasi za kutosha na kumbi za kufanya mikutano pamoja na kutatuliwa changamoto ya ufinyu wa jengo la ofisi za Kamisheni.

TUME YA UTUMISHI WA UMMA

Tume ya Utumishi Serikalini inajukumu la Kusimamia uajiri Serikalini, kuthibitisha, kuachisha na kupendekeza maslahi ya watumishi wa Serikali kwa Kamisheni pamoja na kusikiliza malalamiko ya ajira kutoka taasisi za Serikali.

CHANGAMOTO

1. Tume inakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa nafasi kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Tume.
2. Kamati ilielezwa kuwa Tume haina vitendea kazi muhimu kama vile usafiri. Pia, Kamati ilipofanya ziara katika Tume ya Utumishi wa Umma ilikutana na changamoto ya ukosefu wa usafiri ambapo Tume haina hata gari moja.
3. Ukosefu wa nafasi maalumu za kutunza nyaraka ni changamoto nyengine kubwa ambapo Kamati imezikuta nyaraka nyingi muhimu zimetupwa chini na nyengine kutupwa katika chumba zikiharibika.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaishauri Serikali kuisaidia Tume kupata usafiri angalau gari moja ili iweze kutekeleza kazi zake vizuri.
2. Kamati inaagiza hatua za haraka zichukuliwe kuzikusanya na kuzitunza vizuri nyaraka zilizotupwa katika Afisi za Tume.
3. Kamati inashauri Tume ipatiwe nyongeza ya nafasi za Ofisi kwani watendaji wa Tume wamebanana katika Ofisi moja hali ambayo inazorotesha utendaji wa kazi.

IDARA YA NYARAKA NA KUMBUKUMBU ZA TAIFA

Idara ya nyaraka ni miongoni mwa idara nyeti za Serikali yenye jukumu la kutunza na kuhifadhi kumbukumbuza taifa.
Kamati katika kazi zake za kawaida ilipata nafasi ya kufanya ziara kisiuwani Pemba mabapo ilipokea taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha Julai /Septemba na kuelezwa mambo mbali mbaliya utendaji ambayo mengine yamefikia hatua nzuri na mengine yamekwama kutokana na changamoto mbali mbali zilizopo katika Idara hiyo.

CHANGAMOTO ZA IDARA YA NYARAKA NA KUMBUKUMBU ZA TAIFA

Katika ziara yake kisiwani Pemba. Kamati ilielezwa changamoto zifuatazo:

1. Kamati ilielezwa kuwa Idara kisiwani Pemba inakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa jengo la ofisi ambapo jengo wameshalipata lakini linahitaji kufanyiwa matengenezo makubwa na Idara haina uwezo wa kufanya matengenezo hayo kutokana na ukosefu wa fedha.
2. Idara imeieleza Kamati kuwa upotevu wa nyaraka muhimu za Serikali unasababishwa na baadhi ya watendaji wenyewe ambapo baadhi yao hawatilii maanani umuhimu wa nyaraka hizo hasa wakati wa makabidhiano ya ofisi na wengi wao huona nyaraka hizo hazina maana.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaipongeza Idara ya nyaraka Pemba kwa kuweza kudhibiti nyaraka zake jambo ambalo limepelekea nyaraka kuwa katika hali nzuri na kutopotea kama zilivyopotea Unguja.
2. Kamati inaishauri Serikali kutoa kipaumbele kwaq Idara ya Nyaraka kwa kuwatafutia maeneo yatakayoikidhi mahitaji kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu kwa Unguja na Pemba.
3. Kamati inatoa agizo kwa watendaji wote wa Serikali kuhakikisha kuwa wanazitunza vizuri kumbukumbu muhimu na unapofika wakati wa kuzipeleka Idara ya nyarajka zipelekwe zikiwa salama ili kuzitunza nyaraka hizo kwa matumizi ya baadae.
4. Kamati imesikitishwa na taarifa iliyoipata katika Idara huko kisiwani Pemba kuwa lilitoka agizo la kuhakikisha kuwa afya za wafanyakazi wote wa Idara ya nyaraka zinachunguzwa ambapo barua ilipelekwa Wizara ya Afya kwa utekelezaji wa agizo hilo kutoka Serikalini ambapo bvarua hiyo ilipelekwa mwezi wa March, 2014 lakini hadi hii leo zoezi hilo halijaanza kufanyika. Kutokana na taarifa hiyo, Kamati imesikitishwa sana na taarifa hiyo na inatoa agizo kuwa zoezsi hilo litekelezwe hasa kutokana na mazingira hatarishi ya kazi zinazofanyika katika Idara hiyo.

IDARA YA USALAMA NA AFYA KAZINI

Idara ya usalama na afya kazini injha jukumu la kutoa miongozo ya kuweka mazingira bora ya usalama na afya kazini. Katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi ilifanya ziara katika Idara hii huko kisiwani Pemba na kupewa taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha Julai- Septemba ambapo Kamati ilipokea taarifa hiyo na kutoa miongozo na ushauri kwa Idara. Aidha, Kamati ilielezwa changamoto mbali mbali zinazoikabili Idara kwa sasa.

CHANGAMOTO ZA IDARA YA USALAMA NA AFYA KAZINI

Kamati ilielezwa changamoto zifuatazo:

1. Idara kisiwani Pemba inakabiliwa na changamoto kubwa ya ufinyu wa bajeti ambapo bajeti hiyo haitoshelezi kutekeleza majukumu yote yaliyopangwa ya Idara.
2. Pia Kamati ilipokua katika ziara yake kisiwani Pemba ilielezwa kuwa Idara kwa hivi sasa ina changamoto ya kufanya ukaguzi katika taasisi za Serikali na inafanya kazi ya ukaguzi kwa kuangalia usalama wa wafanyakazi katika taasisi binafsi tu kutokana na kutokamilika kwa muongozo wa wafanyakazi wa Serikali ambapo muongozo huo haujakamilika tokea mwaka 2005 sheria ilipoelekeza hivyo.

MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Kamati baada ya kufanya ziara ilitoa maoni na ushauri ufuatao kwa Serikali:

1. Kamati inazidi kusisitiza suala la kuzishirikisha taasisi za Pemba katika maandalizi ya bajeti na kuhakikisha kuwa taasisi hizo zinapatiwa fedha zilizotengwa katika bajeti ili ziweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu.
2. Kamati ilisikitishwa na taarifa kuwa taasisi za Serikali hadi hivi sasa hazifanyi ukaguzi maofisini kutokana na kutokamilikwa kwa muongozo wa wafanyakazi tokea mwaka 2005, hivyo inatoa agizo muongozo huo ukamilishwe ili taasisi za Serikali ziweze kukaguliwa na kupewa miongozo inayofaa.
3. Kamati inaiagiza Idara ihakikishe kuwa inatoa elimu kwa taasisi za umma kuhusiana na umuhimu wa kuweka mazingira bora na salama maofisini ili wafanyakazi waweze kutekeleza majukumu yao katika hali ya kuridhisha.
4. Kamati inaishauri Serikali iifanyie marekebisho Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2011 kutokana na sheria hiyo kubeba majukumu makubwa na kusababisha mkanganyiko kwa baadhi ya sheria zilizopitishwa hapo awali na kusababisha ugumu katika utekelezaji wa sheria hizo.

IDARA YA MAFUNZO NA MAENDELEO YA RASILIMALI WATU

Idara ya mafunzo na rasilimiali watu ni miongoni mwa idara nyeti ambapo ina jukumu la kuratibu mafunzo ya watumishi wa . Kamati katika ziara yake kisiwani Pemba ilipata taarifa ya Idara hii pamoja na kuelezwa changamoto mbali mbali zilizopo katika idara hii.

CHANGAMOTO ZA IDARA YA MAFUNZO NA RASILIMALI WATU

Idara inakabiliwa na changamoto mbali mbali, miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na:

1. Idara inakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti ambapo inashindwa kutekeleza shughuli zake ilizojipangia kutokana na ukosefu wa fedha.
2. Kamati ilielezwa kuwa Idara ina changamoto ya ukosefu wa vifaa vya ofisi ambapo Idara ina meza na kiti tu. Aidha Kamati ilipatiwa taarifa kuwa Idara haina ofisi yake na wakati Kamati ilipofanya ziara kisiwani Pemba ilielezwa kuwa Idara tatu tofauti zinatumia chumba kimoja kwa ajili ya matumizi ya ofisi.

MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inazidi kusisitiza suala la ushirikishwaji wa Idara za Pemba katika maandalizi ya bajeti pamoja na kuingiziwa fedha za bajeti zilizopangwa.
2. Kamati inaishauri Wizara kufanya nutaratibu wa kuitafutia Idara ofisi yake pamoja na wafabyakjazi kutokana na taarifa kuwa Idara kisiwani Pemba inja mtumishi mmoja na msaidizi alipelekwa muda mfupi kiabla Kamati haijafanya ziara. Hivyo, Kamati inaishauri Wizara iwe *"serious"* kwa kuhakikisha kuwa inaweka wafanyakazi wa kutosha wataosaidia kukamilika kwa majukumu yta idara kwa wakati.

IDARA YA AJIRA

Idara ya ajira ni miongoini mwa idara muhimu kwa maslahi ya wananchi ambayo ina jukumu la kuwaunganisha wananchi wanaotafutakazi na kuwaunganisha na waajiri.
Katika ziara zake kisiwani Pemba, Kamati ilipewa taarifa ya utekelezaji wa bajeti pamoja utekelezaji wake ambapo changamoto kubwa iliyokuwepo kwa iDra zoto nza Pemba ni ukosefu wa fedha kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya malengo yaliyopangwa katika taasisi hizo.

CHANGAMOTO ZA IDARA YA AJIRA

Kamati ilielezwa changamoto zifuatazo:

1. Changamoto kubwa ni ufinyu wa bajeti na kutoshirikishwa katika uandaaji wa bajeti. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa Idara inakabiliwa na changamoto ya kutoshirikishwa nkatika uandaaji wa bajeti na bajeti yotew inapoingia huchukuliwa na Afisi ya Unguja ambapo kwa mwaka mzima Idara himeingiziwa fedha za mafuta kwa ajili ya kufuatilia kazi wanapozipata.
2. Pia idara inakabiliwa na changamotio ya ukosefu wa usafiri ambapo Idara haina usafiri tokea mwaka 2010 wanaazima gari kwa Kamisheni.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha kuwa inazishirikisha Idara zote za Pemba katika maandalizi ya bajetio na iwaingizie fedha zinazopangwa kwa wakati.
2. Kamati inashauiri Idara itafutiwe usafiri wake ili waweze kufanya kazi zao kwa urahisi na ufanisi mkubwa.

KAMISHENI YA KAZI

Kamisheni ina jukumu la kufanya ukaguzi kwa taasisi mbali mbali na kutoa miongozo kwa waajiri na waajiriwa juu ya umuhimu wa kufauatra sheria za kazi, kusuluhisha na kutoa maamuzi ya kwsi mbalkiu mbali za masuala ya kazi nakadhalika.
Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi ilifanya ziara kisiwani Pemba na kupokea taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha Juali/Septemba ambapo ilielezwa majukumu ya Kamisheni pamoja na hatua ilizochukua na changamotoi zilizopo kwa sasa.

CHANGAMOTO ZA KAMISHENI YA KAZI

1. Ufinyu wa bajeti na ucheleweshaji katika ingizaji wa fedha ni changamoto kubwa inayoikabili kamisheni kisiwani Pemba ambapo kamati ilielezwa kuwa katika robo ya kwanza Kamisheni ya Kazi iliingiziwa fedha mwezi wa mwisho jambo ambalo lilipelekea kwa kazi za Kamisheni zilizopangwa kusimama.
2. Pia Kamisheni inakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa vitendea kazi pamoja na usafiri wa uhakika.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inazidisha juhudi za kusisitiza kuwa ni muhimu kuzishirikisha taasisi na Idara za Pemba katika uandaaji wa bajeti. Aidha, suala la uingizwaji wa fedha kwa wakati kwa Idara za Pemba limekuwa ni changamoto kubwa jambo ambalo linasababisha shughuli kutokamilika katika wakati unaotakiwa, hivyo Kamati inasisistiza suala hilo lifanyiwe marekebisho mara moja.
2. Kamati inaishauri Wizara kufanya utaratibu wa kuitafutia Kamisheni usafiri wa uhakika pamoja na vitendea kazi ili watendaji wake waweze kufanbya kazi zao kwa ufanisi.
3. Kamati inaigaiza Kamisheni kuhakikisha kuwa inawachukulia hatua wale wote watakaobainika kuvunja masharti na matakwa ya sheria za kazi hasa katika maeneo ya mikataba ya kazi ya masaa ili kuondoa tatizo hilo na kufuata sheria zilizopo.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI KWA WIZARA YA NCHI (AR) KAZI NA UTUMISH WA UMMA

1. Kamati imebaini kuwa tatizo kubwa linalozikabili taasisi na idara nyingi zilizopo kisiwani Pemba ni tatizo la ufinyu wa bajeti, kutoingiziwa fedha zilizopangwa kwa wakati pamoja na kutozishirikisha taasisi hizo katika masuala ya uandaaji wa bajeti, hivyo Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha kuwa inalifanyia kazi jambo hilo.
2. Kamati ilipewa malamaiko mkuwa Idara za Pemba hazishirikishwi katika suala zima la ziara za kimasomo na badala yake ni idara na taasisi za Unguja tu ndio zinazonufaika na ziara hizo. Hivyo, Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha kuwa inazishirikisha taasisi zote kati8ka ziara za kimasomo mili ziweze kunufaika na ziara hizo.

3. Kamati ilipofanya ziara kisiwanbi Pemba ilisikitishwa na taarifa kuwa Katibu Mkuu wa Wizara kisiwani Pemba tokea kuchaguliwa kwake amefanya ziara siku moja tuu, hivyo, Kamati inamuagiza Katibu Mkuu wa Wizara ya Nchi (AR) Kazi na Utumishi wa Umma anafanya ziara kisiwanin Pemba na kwenda kusikiliza matatizo yaliyopo ya watendaji wake.
4. Kamati inaishauri Wizara kuweka vipaumbele katika maandalizi ya bajeti yake na kuhakikisha kuwa anagalau inazipatia uafiri baadhi ya taasisi ambazo zina matatizo ya usafiri kwa muda mrefu.

SEHEMU YA TATU

HITIMISHO

Katika kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar, Kanuni za Baraza la Wawakilishi na Sheria nyenginezo, Kamati imetoa maelekezo na ushauri wake ambao tunaamini kuwa utasaidia katika kuleta ufanisi kwenye utekelezaji wa majukumu ya Serikali kupitia Wizara ya Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, Wizara ya Katiba na Sheria na Wizara ya Nchi (AR0 Kazi na Utumishi wa Umma. Maelekezo na maoni hayo yalitolewa na Kamati kwa dhamira ya kuwawakilisha vyema wananchi wa Zanzibar na kuona kuwa maslahi ya wananchi hao kwa mujibu wa sheria yanapewa kipaumbele. Kamati yetu inatumai kuwa maelekezo na maoni yaliyotolewa na Kamati kwa Wizara hizo yatazingatiwa kwa lengo la kutoa huduma zilizotukuka kwa wananchi wa Zanzibar.

Kamati inatoa shukurani za pekee kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi, Katibu wa Baraza la Wawakilishi na watendaji wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwanza kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake vizuri, lakini zaidi kwa ushauri walioupatia Kamati yetu katika kipindi cha utekelezaji wa majukumu yake.